# DOUBLE MERIT JARIBIO LA MTIHANI
# DARASA LA SABA - MWAKA 2021
# KISWAHILI

**2ND MERIT**

## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukishachagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala si katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu: -

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni pa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali:**
**<u>Kutoka swali 16 hadi 30 chagua jibu sahihi.</u>**

23. Neno cherehani lina silabi ngapi?

    A. 8
    B. 5
    C. 6
    D. 4

**Jibu sahihi ni D.**

**20.** [A] [B] [C] [D     **21.** [A] [B] [C] [D]     **22.** [A] [B] [C] [D]     **23.** [A] [B] [C] ~~[D]~~

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 23 , kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

***Tumia msamiati ulio mwafaka zaidi ujaze kwenye vihasho 1 hadi 15.***

Ni kweli kwamba jinsi tunavyoendelea kukua ndivyo ___1___ kujifunza mambo mengi aushini. ___2___ ya hayo ni kazi. Kazi ndiyo ___3___ wa maisha ya binadamu. Kazi ni kazi, iwe ya ___4___ au rahisi; usichague. Kwani kazi ___5___ hutusaidia ___6___ riziki yetu. Tujizoeshe, tupende na ___7___ kazi mapema. Wajibu ___8___ nyumbani ni kuwasaidia wazazi katika kazi zote. Ubwete haufai ___9___ hauwezi kutulisha. Tuchape kazi kwanza ___10___ tupumzike.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. tunazidi | B. tunapozidi | C. tunavyozidi | D. tunakozidi |
| **2.** | A. Mmojawapo | B. Mojawapo | C. Kimojawapo | D. Umojawapo |
| **3.** | A. uti wa mgongo | B. uti wa mkono | C. uti wa kichwa | D. uti wa mguu |
| **4.** | A. suluhu | B. sulu | C. zulu | D. sulubu |
| **5.** | A. ndicho | B. ndiyo | C. ndilo | D. ndio |
| **6.** | A. kusumbua | B. kuzubua | C. kuzumbua | D. kusafirisha |
| **7.** | A. kuendeleza | B. kuendelesha | C. kuendelea | D. kuendeleshwa |
| **8.** | A. yetu | B. zetu | C. letu | D. wetu |
| **9.** | A. na | B. wala | C. ingawa | D. lakini |
| **10.** | A. ndiyo | B. ndio | C. ndipo | D. ndiko |

Je ___11___ wajua kuwa ni haki ya kila mtoto kupata elimu? Ni kwa kutambua jambo hili ___12___ serikali ya Kenya ilitangaza kuwa itatoa elimu bila malipo kwa watoto wote ili kila ___13___ apate nafasi ya kujipatia elimu ya msingi. Hali kadhalika watoto wa ___14___ wa kwenda shule hawapaswi kuajiriwa mahali ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. , | B. ? | C. ! | D. . |
| **12.** | A. ambako | B. ambao | C. ambaye | D. ambapo |
| **13.** | A. moja | B. mmoja | C. mamoja | D. mojawapo |
| **14.** | A. rika | B. wakati | C. umri | D. muda |
| **15.** | A. pote | B. kokote | C. popote | D. kote |

**_Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo._**

**16.** Sentensi;

Nilipigiwa mpira ina maana zifuatazo isipokuwa ________


A. mpira ulipigwa ukielekezwa kwangu

B. nilisaidiwa kupiga mpira

C. nilipigwa kwa sababu ya mpira

D. mpira ulitumiwa kunipiga

**17.** Umbo hili ni



A. mstatili

B. mche

C. duara dufu

D. pia

**18.** Neno "maji" liko katika ngeli gani?

A. I-I

B. YA-YA

C. I-ZI

D. LI-YA

**19.** Kamilisha methali:

Mchumia juani

A. hulia kivulini

B. hali wali mkavu

C. huumiza mkonowe

D. marejeo ni ngamani

**20.** Chagua umoja wa sentensi hii:

Watajiwakilisha wao wenyewe

A. Nitajiwakilisha sisi wenyewe

B. Atajwakilisha wewe mwenyewe

C. Nitajiwakilisha mimi mwenyewe

D. Atajiwakilisha yeye mwenyewe

Double Merit Publishers

**21.** Petro alitia ________masomoni na akuibuka mwanafunzi _____ zaidi.

A. chumvi, mzuri

B. bidii, upya

C. fora, bora

D. kauri, kauli

**22.** Msichana alitumia _____ kulia vibanzi.

A. umma

B. uma

C. kijiko

D. mwiko

23. Ni sentensi ipi iliyoakifishwa vizuri?
A. Nilinunua sukari, chumvi, mayai, biskuti
B. Baba wa Wambui ni karimu
C. Lo! Ameshindwa kufunga bao!
D. Mji wa Mombasa unapendeza

24. Ni vazi gani lisilovaliwa na wanaume?
A. Chupi
B. Kizibao
C. Fulana
D. Kanchiri

25. Andika kwa wingi
Mama yake alipoteza ufunguo.
A. Mama zao walipoteza funguo
B. Wamama wao walipoteza funguo
C. Kina mama zao walipoteza funguo
D. Mama zetu walipoteza funguo

26. Chagua kiunganishi katika sentensi hii.
Nilifika sokoni ijapokuwa nilichelewa.
A. sokoni
B. nilifika
C. ijapokuwa
D. nilichelewa

27. Tambua kimilikishi katika sentensi ifuatayo:
Tulimkuta mlevi akiwa amelala nyumbani kwake.
A. mlevi
B. kwake
C. nyumbani
D. amelala

28. Mnyama wa porini anayefanana na ng'ombe ni
A. swara
B. twiga
C. pundamilia
D. mbogo

Double Merit Publishers

29. Kalamu yangu _________ jana.
A. iliibiwa
B. iliiba
C. iliibwa
D. uliibwa

30. Kifaa cha ufundi kinachotumiwa kukerezea mbao ni
A. msumeno
B. patasi
C. nyundo
D. timazi

***Soma kisa kifuatacho kisha ujibu swali 31 hadi 40.***

Siku ya kurudi shuleni iliwadia wazazi wa Pendo waliandamana naye kurudi shuleni. Ulikuwa mwisho wa mwezi na magari ya abiria yalijaa pomoni. Hata hivyo, walifika shuleni salama salimini. Pendo alikuwa amejawa na soni usoni. Hakutaka kumwona yeyote pale shule hasa wanafunzi. Hata hivyo alijikaza kwani alimaizi kuwa lisilobudi hutendwa.

Walimu walimweleza mzazi wa Pendo vile mwanao alivyopotoka zaidi ya kuwa na vipawa adimu. Waliwaeleza pia kuhusu Maria. "Huyu mtoto wa kitajiri ndiye anayempotosha Pendo. Ni lazima aachane naye kabisa ili afaulu katika maisha ya baadaye." Mwalimu mkuu alisema.

Babake Pendo aliposikia jina Maria likitajwa alianza kutafakari. "Mbona jina hili si geni kwangu?" Alijisaili moyoni. Jina hilo lilifanana na la mtoto wa mwajiri wake hata ingawa majina hufanana. Hakuona uwezekano wa mtoto wa mwajiri wake kuwa ndiye aliyemharibu mwanawe. Vilevile, hakuona kama kuna uwezekano kuwa mtoto wa tajiri angesomea hapo.

Musa, babake Pendo, hakujua alikosomea mtoto wa mwajiri wake. Hata hivyo, fikra na jina hilo zilimtatiza kwa muda baba mtu. Baada ya muda mfupi kupita, Musa alimuuliza mwalimu jinsi ya kumsaidia Pendo. Mwalimu mkuu alieleza kwamba jambo hilo lingesuluhishwa vizuri kwa kuwahusisha wazazi wa Maria.

Mwalimu alielezea kwamba wazazi wa Maria walikuwa mabwanyenye katika mitaa ya kifahari. Dhahiri shahiri kuwa haingekosa kuwa yule alikuwa mwajiri wake. Hakutaka mwalimu ajue hivyo licha ya kuwa hisia zake zilidhihisha mengi.

Mwishowe waliagana kwamba Pendo alipaswa kusauriwa na mwalimu na angeripoti katika ofisi ya mwalimu kila alasiri. Pia alipaswa kuadhibiwa kwa kosa lake la kutoroka na ashauriwe barabara na mwalimu kabla ya kwenda kulala.

31. Magari yalijaa pomoni kwa nini?
A. Ilikuwa siku ya kurudi shuleni
B. Ilikuwa asubuhi
C. Ni kawaida ya magari kujaa
D. Ulikuwa mwisho wa mwezi

32. Pendo alirudi shuleni
A. kwa hiari yake
B. siku ya kufungua shule
C. kwa furaha mpwitompwito
D. shingo upande

33. Pendo alikuwa nyumbani kwa sababu
A. ulikuwa mwisho wa mwezi
B. ulikuwa wakati alikizo
C. alitumwa nyumbani kwa utovu wa nidhamu
D. alitaka kuja shuleni ma mzazi wake

34. Maisha ya baadaye ni maisha gani?
A. Maisha ya kisogoni
B. Maisha ya masomo
C. Maisha yajayo
D. Maisha ya furaha

35. Pendo alisomea shule ya aina gani?
A. Ya malazi
B. Ya wavulana na wasichana
C. Ya wasichana pekee
D. Ya kutwa

36. Kwa nini Musa hakutaka wazazi wote wahusike kutafuta suluhisho?
A. Wazazi wa Maria hakujulikana
B. Walikuwa ndio waajiri wake
C. Wangetumia wakati mwingi
D. Wazazi wa Maria walikuwa bwanyenye

37. Neno <u>bwanyenye</u> lina maana gani?
A. maskini hohehahe
B. mti anayeajiri wengine
C. mtu mkubwa serikalini
D. Mtu mwenye mali mengi

38. Pendo alikuwa amefanya kosa gani?
A. Hatujaambiwa
B. Kupigana
C. Kutoroka shuleni
D. Kupendana ma Maria

39. Ni jambo gani Pendo alipaswa kutenda?
A. Kusauriwa kila siku
B. Kuadhibiwa
C. Kutumwa nyumbani
D. Kuachana ma marariki wote

40. Hisia za Bwana Musa zilidhihirisha nini?
A. Kwamba mtoto alikuwa na shida
B. Kwamba alimjua mzazi wa Maria
C. Kwamba Pendo alikuwa hajafanya kosa
D. Kwamba mtoto angeadhibiwa

Double Merit Publishers

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 had 50.</u>**

Ni wazi kama jua la mtikati kuwa demokrasia katika nchi yetu ya Kenya imekua kwa kiwango kikubwa. Bila shaka hili ni suala la kujivunia kwani inamaanisha kuwa tunaenda na wakati. Demokrasia ni mfumo wa kuendesha serikali iliyochaguliwa na watu kwa manufaa ya watu wenyewe. Tangu tulipojinyakulia uhuru yapata miongo mitano iliyopita, nchi yetu imepiga hatua kubwa katika ulingo wa kisiasa.

Rais wa kwanza wa taifa letu tukufu hayati Mzee Jomo Kenyatta aliposhika hatamu za uongozi, alihakikisha kuwa amewaunganish wananchi wote wa taifa hili na kuwapa sababu tosha ya kuionea fahari nchi yao. Aliasisi falsafa ya Harambee ambao ulikuwa mwito wa kuwahamasisha wananchi kushirikiana na kuchangia maendeleo yao kwa kuvuta pamoja. Mwito huo ulileta ari na mshawasha kwa wananchi wa Kenya na kuwahimiza wafanye kazi kwa bidii ili kuinua uchumi wa nchi yao.

Aliposafiri kwa njia ya marahaba mnamo mwaka wa elfu moja mia tisa sabini na nane, hayati rais Daniel Toroitich Arap Moi alishikilia uzi huo huo na kuanzisha mwito wa Nyayo ambao ilimaanisha ya kuwa angefuata nyayo za mtangulizi wake na kuhimiza Wakenya kuishi kwa amani, upendo na umoja.

Hayati Rais Moi alikaa kwenye kiti cha enzi kwa miaka shirini na minne. Ijapokuwa <u>hakuna kapa isiyokosa usubi</u>, alifanya mengi ya kujivunia pia. Hatimaye Rais Mwai Kibaki ambapo Kenya ilijipatia Katiba mpya ambayo hadi sasa imebadilisha sura ya uongozi katika nchi yetu. Kuna mabadiliko mengi ambayo yamejidhihirisha waziwazi hususan katika ulingo wa kisiasa, siyo jinsi mambo yalivyokuwa katika miaka ya awali.

Kwa mujibu wa katiba ya sasa, wakati wa uchaguzi mpiga kura atahitajika kuwachagua viongozi zaidi ya watano. Atahitajika kumchagua rais, gavana wa jimbo lake, seneta, mbunge, mwakilishi wa wanawake bungeni na mwakilishi wa baraza la jimbo. Kwa ujumla, inatazamiwa kuwa katiba hii itaibua viwango vya hali ya juu vya uwajibikaji <u>miongoni mwa</u> wanasiasa na wale wote walio katika nafasi za uongozi.

41. Kidemokrasia, viongozi wa serikali hupigiwa kura na kuchaguliwa na _______ wa nchi husika.
A. wabunge
B. watu
C. wazalendo
D. raia

42. Kiongozi mkuu kabisa wa nchi ambayo ni jamhuri na huchaguliwa kidemokrasia ni
A. Gavana
B. Waziri mkuu
C. Rais
D. Mfalme

43. Ni kauli ipi si sahihi kwa mujibu wa kifungu?
A. Kenya imekuwa nchi huru kwa zaidi ya miaka hamsini
B. Kenya ilijinyakulia uhuru wake mwaka wa hamsini
C. Rais wa kwanza na wa pili kwa sasa hivi ni hayati
D. Kenya tuliadilisha katiba waskati wa Rais Mwai Kibaki

44. Katika aya ya pili, mwandishi hatudokezei kuwa
A. Hayati Mzee Jomo Kenyata aliwapa wananchi wa Kenya sababu tosha ya kuionea fahari nchi yao
B. Hayati Daniel Toroitich Arap Moi aliaga mwa wa elfu moja mia tisa sabini na nane
C. Rais Moi alianzisha kauli mbiu ya kufuata nyayo za Mzee Kenyatta
D. Mwito wa Harambee ulianzishwa

45. Msemo "................... Aliposafiri njia ya marahaba .........." haumaanishi?
A. alipoaga
B. aliposafiri jongomeo
C. alipofariki
D. alipoenda na kucheza ngoma

46. Kulingana ma kifungu
A. Hayati rais Moi aliongoza nchi ya Kenya kwa zaidi ya miongo miwili
B. Kauli mbiu ya Harambee ilihimiza Wakenya kutoishi kwa amani, upendo na umoja
C. Rais Kibaki alibadilisha sura ya uongozi
D. Katiba mpya imeibua maswala mengi mazito

47. Methali nyingine yenye maana sawa na "Hakuna kapa isiyokosa usubi" ni
A. hakuna kovu la masimango
B. hakuna masika yasiyokuwa na mbu
C. kila shetani na mbuyu wake
D. haba na haba hujaza kibaba

48. Nchi ya Kenya ilipatia uhuru mwaka wa
A. 1973
B. 1964
C. 1963
D. 1978

49. Katika aa ya mwisho tunadokezewa ya kwamba
A. mpiga kura atapiga kura kuwachagua viongozi watano
B. katiba mpya itaibua viwango vya ajabu
C. bunge litakuwa na wawakilishi wa wanawake
D. rais, makamu wake, spika na seneta ni baadhi ya viongozi wa serikali ambao watachaguliwa wakati wa uchaguzi

50. Neno <u>miongoni mwa</u> limepigwa mstari katika ufamu liko katika kitengo kipi cha sarufi?
A. Kihisishi
B. Kihusishi
C. Kiunganisho
D. Kivumishi